

**KWENDA: MWENYEKITI, KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**KUTOKA: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

TAREHE: 9 Februari, 2022

**YAH: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA
MWEZI JANUARI, 2022.**

A: MAPATO:

**I. VYANZO VYA MAPATO YA NDANI VYA HALMASHAURI (OWN
SOURCES)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilijiwekea lengo la kukusanya mapato ya **Tzs 9,106,108,000**. Kwa kipindi cha mwezi Januari, 2022 zimekusanywa **Tzs 1,061,335,474.48** sawa na asilimia **11.65** ya Lengo kwa Mwaka. Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Januari 2022 imeweza kukusanya Jumla ya **Tzs 5,497,685,463.43** sawa na asilimia **60.37** ya lengo la mwaka.

Taarifa mlingano ya mwezi Januari, 2022

Lengo la Halmashauri kwa mwezi Januari, 2022 ni kukusanya kiasi cha **Tzs 758,842,333.31** ambapo zimekusanywa **Tzs 1,061,335,474.48** sawa na asilimia **139.86** ya lengo la mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatea ni mchanganuo wa mlingano wa

Mapato halisi kwa mwezi Januari, 2022 kama yalivyokusanywa.

Jedwali la Mlingano: Disemba 2021-Januari 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pun gufu, 2020	(%)
1	Disemba	758,842,333.51	706,908,186.69	(51,934,146.62)	93.16
2	Januari	758,842,333.51	1,061,335,474.48	302,493,141.17	139.86

Ongezeko la ukusanyaji kwa mwezi Januari 2022 limetokana na ukweli kuwa, ni mwezi wa makusanyo ya juu (high season) kwa chanzo cha ushuru wa huduma robo ya pili kimekusanywa mwezi Januari 2022.

II RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilikisia kupokea Ruzuku kutoka Serikali Kuu jumla ya **Tzs 32,818,771,000.00**. Kwa mwezi Januari, 2022 fedha zilizopokelewa ni **Tzs 2,215,332,449.68** sawa na asilimia **6.75** ya bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha Halmashauri ilitarajia kupokea jumla ya **Tzs 2,734,897,583.33** kwa mwezi, ambapo kiasi kilichopokelewa ni **Tzs 2,215,332,449.68** sawa na asilimia **81.00** ya makisio ya mwezi; Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Januari, 2022 imeweza kupokea Ruzuku toka Serikali Kuu Jumla ya **Tzs 15,953,003,869.04** sawa na asilimia **48.61** ya lengo la mwaka.

Ruzuku iliyopokelewa kwa mwezi Januari, 2022 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

JUMLA YA MAPATO YA RUZUKU: Disemba 2021 - Januari , 2022

N a	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pungufu,	(%)
1	Disemba	2,734,897,583.33	2,448,359,320.32	(286,538,263.01).	89.52
2	Januari	2,734,897,583.33	2,215,332,449.68	(519,565,183.65)	81.00

Fedha za ruzuku zilizopokelewa ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa Shule za Msingi na Sekondari, MDH na TASAF.

B: MATUMIZI:

Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Juni 2022 Halmashauri imekisia kutumia **Tzs. 41,924,878,999.76** kati ya fedha hizo **Tzs 32,818,771,000.00** ni kwenye maeneo ya Ruzuku; na **Tzs. 9,106,108,000.00** ni katika maeneo yasiyo ya Ruzuku.

Matumizi halisi kwa mwezi Januari, 2022, ni **Tzs 2,556,666,936.07** sawa na asilimia **6.09** ya jumla ya matumizi ya fedha. Jumla ya matumizi yote ya ruzuku kwa Mwezi Januari, 2022 ni **Tzs 2,174,960,854.71** sawa na asilimia **6.62** ya lengo la mwaka.

Matumizi ya vyanzo vya ndani kwa mwezi Januari, 2022 ni **Tzs 381,706,081.36** sawa na asilimia **4.19** ya bajeti ya matumizi ya fedha za mapato ya ndani. Aidha Halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Januari, 2022 imeweza kutumia jumla ya **Tzs 18,938,395,760.38** sawa na asilimia **45.17** ya lengo la mwaka.

Mchanganuo wa matumizi ya Fedha Mwezi Januari, 2022 ni kama ifuatavyo:

▪ Matumizi maeneo yasiyo ya ruzuku	Tzs	381,706,081.36
▪ Matumizi maeneo ya Ruzuku	Tzs	2,174,960,854.71
Jumla	Tzs	2,556,666,936.07

Matumizi yaliyofanyika ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa elimu msingi na sekondari, MDH, TASAF, Mfuko wa pamoja wa Afya (Basket fund) na matumizi ya vyanzo vya mapato ya ndani.

Matumizi ya fedha zilizopokelewa nje ya bajeti kwa mwezi Januari 2022 ni **Tzs 2,640,000.00** kwa ajili ya shughuli za uratibu wa chanjo ya UVIKO 19

Jedwali "A", "B" "C" na "D" ikionyesha muhtasari Mapato, Matumizi, mchanganuo wa taarifa mlingano wa mapato ya ndani wa mwezi Januari, 2022 na mchanganuo wa matumizi (itemized),

Nawasilisha,

Mwamtobe U.E
**K.N.Y: MKURUGENZI WA MANISPAA
 HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**